

Jina..... Nambari ya usajili...../.....

Shule..... Tarehe .....

Sahihi ya Mtahiniwa.....

102/2

**KISWAHILI**

**Karatasi ya 2**

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu jamii)

**JULAI / AGOSTI - 2012**

**MUDA: SAA 2 ½**

**MTIHANI WA TATHMINI WA PAMOJA WA WILAYA YA KWANZA- 2012**  
**Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari**

**Maagizo**

1. Jibu maswali yote
2. Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Swali	Alama	Tuzo
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
<b>Jumla</b>	80	

*Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa*

*Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

**Soma kifungu hiki kasha ujibu maswali.**

Binadamu heshi kuwa na falsafa zinazojiri akilini mwake. Amejichanjia kijisayari chake na kufikirika mfano wa Mirihi katika falaki yake ya maisha. Ni sayari ndogo ambayo imejitenga na sayari nyingine kama vile kausi.

Mirihi kuna viumbe mauluti vyenye mitindo ya kustaajibisha. Tofauti na Kausi ambayo ambako mabinti huwa na urembo wa kiasilia, wanamirihi ni “warembo” mithili ya walioanguliwa ja vifaranga. Viganja vyao na nyuso zao huwa zimekandwa kwa mafuta ya zebaki zikawa nyororo japo wengi huwa mithili ya suriama. Wasalaminiapo na Wanakausi mikwaruzo yao huwachipua ngozi kwa kazi ya sulubu waifanyayo shambani. Fauka ya uhotara huo, wamefungasha kiasi huku wamejisetiri kwa vijisuruali na vijisketi ambavyo vimewabana kana kwamba vimeundwa kwa vitambaa vya mikononi na kutafuta misada kutoka kwa majirani kuvivua na kuvivaa

Wanakausi waliovalia nguo zinazowafika kwenye visigino, huchushwa mno na hivi vijiguo vinavyowasetiri hadi kwenye sisemi vilegesambwa, ukipenda magotini, bali kwenye mapaja. Ni kweli kwamba waso haya wana mji wao. Wanapondatia hasa kwenye hafla za maziko au arusi katika sayari ya Kausi Wanakausi hujibana pembeni kujionea malimweng ulimwenguni. Minong’onezo ndio itajaa hewani “ ni yakini Pemba ndiko kwenye nguo na wenda uchi wapo”

Katika hafla hizo, wale mabinti wazuri wa Mirihi hubeba **vibogoshi** ambamo mara kwa mara hutoa vidubwasha vidogo vidogo na kuendelea kujipodoa huku shughuli zinapoendelea. Pengine huenda umesahau kuwa katika mipango na makadirio ya matumizi ya hafla hiyo marejeleo yanayokaririwa huwa “...wajua watu wa Mirihi hawapendi.....”

Mabinti wazuri wa Mirihi kila mmoja huwa amejibebea mwavuli na kujizuia mvua au jua huku amekumbatia maji ya chupa ya kutoka kwenye ya Mirihi.

Wanakausi walalahoi huwa wakikata kiu yao rahisi kutoka kwenye mapipa yaliyojazwa maji au kwenye mifereji waliyobahatika kuwekewa na wizara ya maji, kwa kutumia viganja vya mikono. Mabwana wa Mirihi hawana haja na miavuli, wao huwa watu wenye zao. Huvalia kofia nene zinazoonekana kama somberero. Watembeapo huning’iniza funguo za magari ya kifahari katika mkono wa kushoto na simu ya rununu katika mkono wa kulia

Hapa na pale watakuwa wakiwasiliana kwa simu zao na pia kupiga gumzo na maghulumu wa Kausi ambao kwa kawaida watakuwa wakiwarai Wanamirihi, “**Utaniacha hivyo**”

Baada ya hafla, mlo ambao huwa Wanamirihi hupakukuliwa huku Mabwanamirihi wakidakia wasichelewe, mabintimirihi wakinyofoa kwa mikono au kung’ofoa kwa midomo yao myekundu na Wanakuasi wakichungulia kwa mbali wakisubiri nafasi yao itimie.

Ghafla mawingu yataanza kutanda upande wa mashariki na mambo sasa yatachukua mkondo mpya. Wanamirihi mchakamchaka huengaenga, mbio kwenye magari yao. Lakini kuna wale ambao

hawana magari ya kukimbilia. Kawaida yao huyaita Wanamirihhi wenzao faraghani “Baba fulani umejaza?”

Wengine hubaki kusema, “Uenda basi letu likianiacha, tutaonana nikija wikendi.”

Hali iwapo mwanana, Wanakausi watakuwa sasa ndio wakati wa kujitambulisha na wengine kuyajaza magari ya Wanamirihhi ya kifahari kwa maembe, avokado, ndizi na makochokocho ya vitu vya shambani. Baada ya miezi kadha, Wanakausi wachache watawazuru Wanamirihhi kuwapa shukurani katika kijisayari chao cha Mirihhi.

Hapo sasa watawumbua jibu la kitendawili watakapokumbana na Bintimirihhi amebeba kijikaratasi cha nailoni kimejazwa embe dondo moja, sukuma wiki, bila kusahau kishemu cha nyama alichopimiwa cha shilingi kumi. Kwa kuwa atapata malazi kwake atamshauri, “.....pengine unionyeshe bucheri tununue nyama. ...pitie dukani tununue.....” hapo kwake Malaika atakuwa ameshuka kutoka Kausi hadi Mirihhi.

Lakini wengine ni wale ambao pindi tu utakapowasalimia watakukwa na “zamu ya usiku siku hiyo.” Wanaovalia somerero watamlaki Mwanakausi kwa mlahaka wa kifalme ili akastaajibie vitu kama **Majirafu**, mazulia, makochi, taja nitaje.

Yule wa awali atalala usiku huo usingizi mnono usio na bugudha na kwenye kochi huku akihimiria kurauka mapema asikutwe na waliolala nyuma ya pazia. Hisia za Mwanakausi zitamrudisha katika tamthilia ya Wole Soyinka “Masaibu ya ndugu Jero kuwa “vidole vyote havikuumbwa sawa.” Mirihhi ni sayari iliyosheheni watu na viatu, kumbe Kausi ni shamba la paukwa na pakawa la Edeni. Tafakari haya.

### Maswali

1. Andika anwani mwafaka ya taarifa hii (Alama 2)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

2. Eleza tofauti kati ya wanawake wa Mirihhi na wale wa Kausi. (Alama 2)

.....  
.....  
.....

3. “Mabwana wa Mirihhi ni watu wenye zao”. Thibitisha. (Alama 3)

For More Free KCSE past papers visit [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

4. Ni dhahiri kuwa Mrihi ni sayari yenye watu na viatu. Nini maana ya viatu. Je, kuna viatu hapa? Thibitisha. (Alama 3)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

5. Mwandishi anamaanisha nini anaposema “Utaniacha hivyo?” (Alama 2)

.....  
.....  
.....

6. Eleza maana ya: (Alama 2)

i) Jirafu

.....  
.....  
.....

ii) Vibogoshi

.....  
.....  
.....

Katiba mpya imeipa lugha ya Kiswahili hadhi nyingine kuifanya kuwa lugha rasmi kando na kuwa ni lugha ya taifa. Mabadiliko haya muhimu yana changamoto kadhaa:

Kwanza kabisa lugha ya Kiswahili sasa itashindania nafasi sawa na ile ya kiingereza katika shughuli za kikazi. Swala hapa linahusu majukumu ambayo lugha hizi zitatekeleza. Je, lugha hizi zitatumika mtawalia katika shughuli za kikazi au zitatengewa majukumu maalum?

Lugha ya kswahili itachukua nafasi ipi? Kiingereza kitaachiwa nani tukizingatia kuwa kwa muda mrefu lugha ya kiingereza ndio imekuwa lugha tawala katika mazingira haya? Je, wananchi wataweza kufanya maombi ya kazi kwa lugha ya Kiswahili kando na kuendesha mawasiliano ya kiofisi kwa lugha hii. Kwa kupi ili kusitokee mgongano wa matumizi ya lugha hizi mbili ni muhimu sana kwa watungasera kueleza kinagaubaga mawanda ya matumizi ya lugha hizi mbili katiaka mazingira ya kikazi.

Changamoto jingine na muhimu ni kiwango cha maandalizi ya wananchi katika kuyapokea mabadiliko haya. Kwanza, wananchi wanafaa wafahamishwe kuhusu haki yao ya kutumia lugha hii katika mazingira ya kazi. Si ajabu kuwa wengi wao hawana habari kuhusu mabadiliko haya ya kisera. Watumishi wa umma nao wanastahili kupewa mafunzo maalum kuhusu mbinu za mawasiliano katika kiswahili waendeshe shughuli zao vizuri.

Kwa upande mwingine, vyyo vikuu pamoja na taasisi nyingine za mafunzo zinastahili kutoa kkozi ya lazima katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojiunga nazo ili kuwaandaa kwa mahitaji haya mapya ya kikatiba. Kadhalika, serikali inastahili kuwanda wataalamu zaidi wa lugha ya Kiswahili ambao watahusika katika kuwafunza wanaohusika na utekelazaji sera.

Kuna haja pia ya wataalamu wa lugha kuandika vitabu zaidi kwa lugha ya Kiswahili ambavyo vitatoa mafunzo kuhusu mbinu mbalimbali za mawasiliano. Shughuli hii iambatane na ile ya kutafsiri vitabu vilivyoandikwa kwa lugha zingine kwa ile ya Kiswahili.

Kwa muda mrefu sasa, kumekuwa na tatizo la mtazamo hasa miongoni mwa wananchi kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wananchi wamekuwa na sababu zao za kutoitumia lugha hii wakishikilia kuwa lugha yenyewe ni ngumu.

Aidha, wananchi wengi wamekuwa na uzoefu wa kuzungumza lugha ya kiingereza au lugha nyingine za kigeni huku wakitoa nafasi finyu kwa lugha ya Kiswahili. Serikali inastahili kutafuta njia ya kuwahimiza wananchi wote kuionea fahari lugha ya kiswahili, waipende na kuielewa vizuri.

Ni muhimu kufanywe kila juhudi kuhakikisha kuwa wananchi wanatumia Kiswahili sanifu ili wasije wakakivuruga kwa kukiendeleza visivyo au kwa kukiharibu kwa kijilugha cha sheng au kw alugha za kienyeji.

Vile vile ni muhimu wananchi watambue kuwa nchi yetu ya Kenya ndiyo kitovu cha lugha hii na hivyo basi wafanye kila juhudi kuitumia ipasavyo ili tusionekane kuwa watumwa katika lugha yetu asili.





**SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA**

**(Alama 40)**

a) Taja sauti mbili ambazo ni vipasuo vya ndomo

(Alama 2)

.....  
.....  
.....

b) Tunga sentensi ya neno moja yenye sehemu zifuatazo

(Alama 3)

- i) Ngeli
- ii) Wakati
- iii) Kirejeshi
- iv) Mzizi
- v) Kauli
- vi) Kiishio

.....  
.....  
.....

c) Taja ngeli za majina yafuatayo

(Alama 2)

- i) Uga

.....  
.....  
.....

- ii) Kiroboto

.....  
.....  
.....

d) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo:

(Alama 2)

- i) Kiwakilishi nafsi kiambata

.....  
.....  
.....

- ii) Kiwakilishi ngeli

.....  
.....  
.....

e) Andika kwa kinyume

(Alama 1)

Kijakazi aliangika vyombo vya tajiri wake.

.....  
.....



f) Unda nomino dhahania kutokana na vitenzi hivi: (Alama 2)

i) Cheza

ii) Pika

.....  
.....  
.....

g) Tunga sentensi sahihi kukbainisha tofauti kati ya maneno haya: (Alama 2)

i) Jua

ii) Juka

.....  
.....  
.....

h) Andika katika ukubwa. (Alama 1)

Sungura ambaye alikatwa mkia aliingia nyumbani.

.....  
.....

i) Tambua shamirisho na chagizo katika sentensi hii. (Alama 2)

Alipiga teke mpira ukaruka juu juu zaidi.

.....  
.....  
.....

j) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (Alama 4)

Mto ule uliofurika jana umezoa taka nyingi.

k) Kanusha. (Alama 1)

Jembe hilo ndilo nitumialo kulima shamba langu.

.....  
.....  
.....

l) Tambua aina za vishazi katika sentensi ifuatayo: (Alama 2)

Mtoto mwenye bidii hufanya vyema.

.....

.....

.....

.....

.....

m) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. (Alama 2)

i) Tua (Tendama)

.....

.....

.....

.....

.....

ii) Fumba (Tendata)

.....

.....

.....

.....

.....

n) Eleza matumizi mawili ya ritifaa na utolee mifano kwa kila moja. (Alama 2)

.....

.....

.....

.....

o) Andika katika usemi wa taarifa. (Alama 2)

“Nitakuja kesho asubuhi. Inshallah!” Bakari alisema.

.....

.....

p) Eleza maana mbili inayotokana na sentensi hii. (Alama 2)

Aliletewa ng’ombe na mtoto wake.

.....

.....

.....

.....

q) Yakinisha. (Alama 2)  
Asiposhiba hatafunguliwa.

.....  
.....  
.....  
.....  
.....

r) Tunga sentensi ukitumia vivumishi vifuatavyo: (Alama 2)

i) 'a' mnganifu

.....  
.....  
.....

ii) Amba-rejeshi

.....  
.....  
.....

s) Sahihisha sentensi hii kwa njia tatu. (Alama 3)

Hapa ndipo alikofia.

.....  
.....  
.....  
.....  
.....

t) Iweke sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu. (Alama 1)

Aliomba msamaha kwa kuchelewa.

.....  
.....  
.....  
.....  
.....

